

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Anuani ya Simu "TAMISEMI" DODOMA  
Simu Na: +255 26 2321607  
Nukushi: +255 26 2322116  
Baruapepe: [ps@tamisemi.go.tz](mailto:ps@tamisemi.go.tz)



Mji wa Serikali – Mtumba,  
Mtaa wa TAMISEMI,  
S.L.P. 1923,  
41185 DODOMA,  
Tanzania.

12 Novemba, 2024

TAARIFA KWA UMMA

**KUONGEZA MUDA WA KUWASILISHA NA KUTOA  
MAAMUZI YA RUFAA ZA WAGOMBEA**

Ninapenda kuutaarifu umma na wadau wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2024 kuwa, kufuatia maoni mbalimbali tuliyopokea kutoka kwa wadau wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa vikiwemo vyama vya siasa kuhusu mchakato wa uteuzi na ushughulikiaji wa pingamizi za wagombea wa nafasi mbalimbali katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa na muda wa kuwasilisha na kutoa maamuzi ya rufaa za wagombea ambao hawakuteuliwa, kwa kuzingatia mamlaka niliyonayo kwa mujibu wa Kanuni ya 52 ya Tangazo la Serikali Na.571,573, 574 na Kanuni ya 50 ya Tangazo la Serikali Na.572 yote ya tarehe 12/7/2024, inayompa Waziri uwezo wa kutoa maelekezo na miongozo mbalimbali kuhusu uchaguzi, ninapenda kutoa mwongozo ufuatao:-

1. Ninaongeza muda wa Kamali za rufani za Wilaya wa kupokea, kusikiliza na kutoa uamuzi wa rufaa iliyowasilishwa kwa muda wa siku mbili zaidi. Hivyo, muda unaongezwa kutoka tarehe 13/11/2024 na sasa rufaa zitapokelewa, kusikilizwa na kutolewa uamuzi hadi tarehe 15/11/2024 saa 12 Jioni. Hivyo, wagombea wote ambao pingamizi zao hazikukubalika wanaweza kuwasilisha rufaa zao mpaka tarehe 15 Novemba, 2024.



Karibu na Mtaa, Kazi ya Wenzetu  
Jitihada Wazihitaji Uchaguzi

2. Ninazielekeza kamati za rufani za Wilaya kuitisha fomu za wagombea wote walioenguliwa/hawakuteuliwa ili kufanya mapitio na kujiridhisha na sababu zilizopelekea wagombea hao kutoteuliwa ili haki iweze kutendeka kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Uchaguzi.
3. Ninawaelekeza wasimamizi wa uchaguzi katika Halmashauri zote kuwarejesha wagombea wa vyama vyote ambao walienguliwa kwa sababu ya kutodhaminiwa na vyama vyao katika ngazi ya Kijiji/Mtaa pamoja na kuwa vyama hivyo viliwasilisha barua za kuainisha ngazi ya chini ya udhamni kuwa ni Kata ikiwemo Chama cha ACT-Wazalendo kilichowasilisha ngazi yake ya udhamini kuwa ni ngazi ya Kata.
4. Ninavihimiza vyama vya siasa ambavyo wagombea wao wameenguliwa kutumia vizuri muda huu wa siku mbili ulioongezwa endapo hawakuridhika na uamuzi wa wasimamizi wasaidizi kuhakikisha wanasimamia wagombea wao waweze kuwasilisha rufaa zao kwa kamati za rufani zilizopo katika kila wilaya husika.
5. Ofisi ya Rais - TAMISEMI itaendelea kuhakikisha inasimamia misingi ya Utawala Bora ikiwemo kuhakikisha wananchi wanapata nafasi ya kuchagua viongozi wanaowataka na kuchaguliwa kushika nafasi mbalimbali za uongozi.
6. Mwisho ninawashukuru wadau wote wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa ushirikiano wao wanaoendelea kuipatia Ofisi hii katika mchakato wa uchaguzi na nitoe wito kwa pande zote ikiwa ni pamoja na wasimamizi wa uchaguzi kuendelea kuzingatia Sheria, Kanuni, na Taratibu ili kuhakikisha mchakato wa uchaguzi unaendelea kuwa wa haki, uwazi na unaozingatia misingi ya demokrasia.



Mohamed O. Mchengerwa (Mb.)  
**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS**  
**(TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)**



Katiba ya Rais, Ofisi ya Waziri wa Nchi,  
250000 Dar es Salaam, Tanzania